# Malaki

1 Neno la unabii: Neno la Mwenyezi Mungu
kwa Israeli kupitia kwa Malaki.

### *Yakobo alipendwa, Esau alichukiwa*

2 Mwenyezi Mungu asema, "Nimewapenda
ninyi.

"Lakini ninyi mnauliza, 'Wewe umetupendaje?' "

Mwenyezi Mungu asema, "Je, Esau hakuwa ndugu yake Yakobo? Hata hivyo nimempenda
Yakobo,
3 lakini nikamchukia Esau, nami nimeifanya
nchi yake ya vilima kuwa ukiwa, na urithi wake
nimewapa mbweha wa jangwani."
4 Edomu anaweza kusema, "Ingawa tumepon-
dapondwa, tutajenga upya magofu."

Lakini hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni: "Wanaweza kujenga, lakini nitabomoa. Wataitwa Nchi Ovu, watu ambao siku zote wapo chini ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.
5 Mtayaona kwa macho yenu wenyewe na
kusema, 'Mwenyezi Mungu ni mkuu, hata nje ya
mipaka ya Israeli!'

### *Dhabihu zilizo na mawaa*

6 "Mwana humheshimu baba yake, naye mtu-
mishi humheshimu bwana wake. Kama mimi
ni baba, iko wapi heshima ninayostahili? Kama
mimi ni bwana, iko wapi heshima ninayostahili?"

asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni. “Ni ninyi, enyi makuhani, mnaolidha-
rau Jina langu.
“Lakini mnauliza, ‘Tumelidharau Jina lako kwa
namna gani?’
7 “Mnatoa sadaka chakula kilichotiwa unajisi
juu ya madhabahu yangu.
“Lakini ninyi mnauliza, ‘Tumekutia unajisi kwa
namna gani?’
“Kwa kusema kuwa meza ya Mwenyezi Mungu
ni ya kudharauliwa.
8 Mnapoleta dhabihu za wanyama walio
vipofu, je, hilo si kosa? Mnapoleta dhabihu
zilizo vilema au wanyama wagonjwa, je, hilo
si kosa? Jaribuni kuvitoa kwa mtawala wenu!
Je, angefurahishwa nanyi? Je, atawakubalia?”
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni.
9 “Basi mwombeni Mungu awe na neema
kwetu. Je, kwa sadaka kama hizo kutoka
mikononi mwenu, atawapokea?” asema
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni.
10 “Laiti mmoja wenu angeifunga milango ya
Hekalu, ili msije mkawasha moto usiokuwa na
faida juu ya madhabahu yangu! Sina furaha
nanyi,” asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa ma-
jeshi ya mbinguni, “nami sitaikubali sadaka toka
mikononi mwenu.
11 Jina langu litakuwa kuu miongoni mwa
mataifa, kuanzia mawio ya jua hata machweo
yake. Kila mahali uvumba na sadaka safi zi-
taletwa kwa Jina langu, kwa sababu Jina langu

litakuwa kuu miongoni mwa mataifa," asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.
12 "Lakini mnalinajisi Jina langu kwa kusema kuhusu meza ya Bwana, 'Imetiwa unajisi pamoja na chakula chake. Ni ya kudharauliwa.'
13 Nanyi mnasema, 'Mzigo gani huu!' Nanyi mnaidharau kwa kiburi," asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

"Mnapowaleta wanyama mliopokonya kwa nguvu, walio vilema au walio wagonjwa na kuwatoa kama dhabihu, je, niwakubali kutoka mikononi mwenu?" asema Mwenyezi Mungu.
14 "Amelaaniwa yeye adanganyaye, aliye na mnyama wa kiume anayekubalika katika kundi lake na kuweka nadhiri ya kumtoa, lakini akatoa dhabihu ya mnyama aliye na dosari kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa mimi ni Mfalme Mkuu, nalo Jina langu linapaswa kuogopwa miongoni mwa mataifa," asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

# 2

### *Onyo kwa makuhani*

1 "Sasa onyo hili ni kwa ajili yenu, enyi makuhani.
2 Kama hamtasikiliza, na kama hamtaki kuielekeza mioyo yenu kuheshimu Jina langu, nitatuma laana juu yenu, nami nitalaani baraka zenu. Naam, nimekwisha kuzilaani, kwa sababu hamkuielekeza mioyo yenu kuniheshimu mimi," Asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

3 “Kwa sababu yenu nitawakatilia mbali wazao
wenu. Nitazipaka nyuso zenu kinyesi, hicho
kinyesi cha dhabihu zenu. Nanyi mtafukuzwa
pamoja nazo mtoke mbele zangu.
4 Nanyi mtajua kuwa nimewapelekea onyo hili
ili agano langu na Lawi lipate kuendelea,” asema
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni.
5 “Agano langu lilikuwa pamoja naye, agano la
uhai na amani, nami nilimpa yote, ili aniche na
kuniheshimu, naye akaniheshimu na kusimama
akilicha Jina langu.
6 Fundisho la kweli lilikuwa kinywani mwake,
wala hakuna uongo wowote uliopatikana katika
midomo yake. Alitembea nami katika amani na
unyofu, naye akawageuza wengi kutoka dham-
bini.
7 “Kwa maana yapasa midomo ya kuhani kuhi-
fadhi maarifa. Tena kutoka kinywani mwake
watu wangepaswa kutafuta mafundisho, kwa
sababu yeye ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni.
8 Lakini mmegeuka mkaiacha njia, na kwa ma-
fundisho yenu mmesababisha wengi kujikwaa.
Mmevunja agano na Lawi,” asema Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.
9 “Kwa hiyo nimewasababisha ninyi kudha-
rauliwa na kufedheheshwa mbele ya watu wote,
kwa sababu hamkufuata njia zangu, bali mme-
onesha upendeleo katika mambo ya sheria.”

### *Yuda si mwaminifu*

10 Je, sote hatuna Baba mmoja? Hatukuumbwa
na Mungu mmoja? Kwa nini basi tunalinajisi
agano la baba zetu kwa kukosa uaminifu kila
mmoja kwa mwenzake?

11 Yuda amevunja uaminifu. Jambo la
kuchukiza limetendeka katika Israeli na
katika Yerusalemu: Yuda amepanajisi mahali
patakatifu apendapo Mwenyezi Mungu, kwa
kuoa binti ya mungu mgeni.

12 Kwa maana kwa mtu yeyote atendaye jambo
hili, Mwenyezi Mungu na amkatilie mbali kutoka
mahema ya Yakobo, hata kama huwa anamletea
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni sadaka.

13 Kitu kingine mnachokifanya: Mnaifurikisha
madhabahu ya Mwenyezi Mungu kwa machozi.
Mnalia na kuugua kwa sababu yeye haziangalii
tena sadaka zenu wala hazikubali kwa furaha
kutoka mikononi mwenu.

14 Mnauliza, "Kwa nini?" Ni kwa sababu
Mwenyezi Mungu ni shahidi kati yako na mke
wa ujana wako, kwa sababu umevunja uaminifu
naye, ingawa yeye ni mwenzako, mke wa agano
lako la ndoa.

15 Je, Mwenyezi Mungu hakuwafanya wao
kuwa mmoja? Katika mwili na katika roho wao
ni wa Mungu. Kwa nini wawe mmoja? Kwa
sababu Mungu alikuwa akitafuta mzao mwenye
kumcha Mungu. Kwa hiyo jihadharini wenyewe
katika roho zenu, mtu asivunje uaminifu kwa
mke wa ujana wake.

16 "Ninachukia kuachana," asema Mwenyezi
Mungu, Mungu wa Israeli, "pia nachukia mtu

anayejivika jeuri kama vazi," asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

Kwa hiyo jihadharini wenyewe katika roho zenu, wala msije mkavunja uaminifu.

### *Siku ya hukumu*

17 Mmemchosha Mwenyezi Mungu kwa maneno yenu.

Nanyi mnauliza, "Tumemchosha kwa namna gani?"

Mmemchosha kwa kusema, "Wote watendao mabaya ni wema machoni pa Mwenyezi Mungu, naye anapendezwa nao" au "Mungu wa haki yuko wapi?"

## 3

1 "Angalieni, nitamtuma mjumbe wangu,
atakayeiandaa njia mbele yangu. Ndipo ghafula Bwana mnayemtafuta atakuja hekaluni mwake. Mjumbe wa agano, ambaye mnamwonea shauku, atakuja," asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

2 Lakini ni nani atakayeweza kustahimili hiyo
siku ya kuja kwake? Ni nani awezaye kusimama atakapotokea? Kwa kuwa atakuwa kama moto wa mfua fedha au kama sabuni ya mfua nguo.

3 Ataketi kama mfuaji na asafishaye fedha.
Atawatakasa Walawi, naye atawasafisha kama dhahabu na fedha. Kisha Mwenyezi Mungu atakuwa na watu watakaoleta sadaka katika haki,

4 nazo sadaka za Yuda na Yerusalemu zitakubalika kwa Mwenyezi Mungu, kama katika siku zilizopita, kama katika miaka ya zamani.

5 “Basi nitakuja karibu nanyi ili kuhukumu.
Nami nitakuwa mwepesi kushuhudia dhidi ya
wachawi, wazinzi, waapao kwa uongo, wanaop-
unja vibarua malipo yao, wanaowadhulumu wa-
jane na yatima, na wanaowanyima wageni haki,
lakini hawaniogopi mimi,” asema Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

### *Kumwibia Mwenyezi Mungu*

6 “Mimi Mwenyezi Mungu sibadiliki. Kwa hiyo
ninyi, enyi uzao wa Yakobo, hamjaangamizwa.
7 Tangu wakati wa baba zenu mmegeukia
mbali na amri zangu nanyi hamkuzishika. Niru-
dieni mimi, nami nitawarudia ninyi,” asema
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni.

“Lakini mnauliza, ‘Tutarudi kwa namna gani?’
8 “Je, mwanadamu atamwibia Mungu? Hata
hivyo mnaniibia mimi.

“Lakini mnauliza, ‘Tunakuibia kwa namna
gani?’

“Mnaniibia zaka na dhabihu.
9 Mko chini ya laana, ninyi taifa lote, kwa
sababu mnaniibia mimi.
10 Leteni zaka kamili ghalani, ili kuwe na
chakula katika nyumba yangu. Nijaribuni
katika hili,” asema Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni, “nanyi mwone kama
sitawafungulia madirisha ya mbinguni na
kuwamwagieni baraka nyingi hata mkose nafasi
ya kutosha.
11 Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye,
wala hataharibu mazao ya ardhi yenu, wala
mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake

kabla ya wakati wake," asema Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni.
12 "Ndipo mataifa yote yatawaita mliobarikiwa,
kwa maana nchi yenu itakuwa ya kupendeza
sana," asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa ma-
jeshi ya mbinguni.

### *Kiburi cha Israeli dhidi ya Mwenyezi Mungu*

13 "Mmesema vitu vigumu dhidi yangu," asema
Mwenyezi Mungu.

"Hata hivyo mnauliza, 'Tumesema nini dhidi
yako?'
14 "Mmesema, 'Ni bure kumtumikia Mungu.
Tumepata faida gani kwa kushika maagizo
yake na kwenda kama waombolezaji mbele za
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni?
15 Lakini sasa wenye kiburi wanabarikiwa.
Hakika watenda maovu wanastawi, pia hata
wale wanaoshindana na Mungu ndio wanaosal-
imika.' "
16 Ndipo wale waliomcha Mwenyezi Mungu
wakasemezana wao kwa wao, naye Mwenyezi
Mungu akasikiliza na akasikia. Kitabu cha
kumbukumbu kikaandikwa mbele yake kuhusu
wale ambao walimcha Mwenyezi Mungu na kuli-
heshimu jina lake.
17 "Nao watakuwa watu wangu," asema
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni, "katika siku ile nitakapowafanya
kuwa hazina yangu ya pekee. Nitawahurumia,
kama vile kwa huruma mtu amhurumiavyo
mwanawe anayemtumikia.

18 Kwa mara nyingine tena utaona tofauti kati
ya wenye haki na waovu, kati ya wale wanaom-
tumikia Mungu na wale wasiomtumikia.

# 4

*Siku ya Mwenyezi Mungu*

1 "Hakika siku inakuja, itawaka kama ta-
nuru. Wote wenye kiburi na watenda maovu
watakuwa mabua makavu, na siku ile inayokuja
itawawasha moto," asema Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni. "Hakuna mzizi
wala tawi litakalosalia kwao.
2 Bali ninyi mnaoliheshimu Jina langu, jua la
haki litawazukia, lenye kuponya katika mabawa
yake. Nanyi mtatoka nje na kurukaruka kama
ndama aliyeachiwa kutoka zizini.
3 Kisha ninyi mtawakanyaga waovu, nao
watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu
siku ile nitakayofanya mambo haya," asema
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni.
4 "Kumbukeni Torati ya mtumishi wangu Musa,
amri na sheria nilizompa huko Horebu kwa ajili
ya Israeli wote.
5 "Tazama, nitawapelekea nabii Ilya kabla ya
kuja siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Mwenyezi
Mungu.
6 Ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto
wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, la
sivyo nitakuja na kuipiga nchi kwa laana."

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: “The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible.”

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d